HOTUBA YA MHE. *KAPT (MST)* GEORGE H. MKUCHIKA (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWENYE UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA WAKUU WA IDARA ZA UTAWALA NA RASILIMALIWATU KATIKA WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA, WAKALA, TAASISI ZA UMMA, SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KATIKA UKUMBI WA CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI (IRDP)

DODOMA – TAREHE 17 OKTOBA, 2018.

Mhe. Seleman S. Jaffo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR- TAMISEMI);

Dkt. Laurean J.P. Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambaye pia ni Mwenyekiti na Mratibu wa Kikao hiki;

Eng. Mussa I. Iyombe, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI);

Ndugu Dorothy Mwaluko, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kikao hiki;

Ndugu Watendaji wa Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

Ndugu Wajumbe wa Kikao;

Wanahabari;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana, **Habarini za asubuhi.**

Ndugu Washiriki,

Awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema kwa kutujalia uzima na kutuwezesha kukutana hapa leo katika kikao hiki muhimu. Pia ninapenda kutoa shukrani kwa Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuandaa kikao hiki chenye lengo la kukumbushana, kupeana maelekezo ya kazi na kuelimishana kuhusu taratibu mpya za utendaji wa kazi katika Utumishi wa Umma zilizopo na zinazotarajiwa kuwepo ili kuimarisha utendaji kazi na kuboresha utoaji wa huduma bora kwa Umma. Kikao hiki pia kinatoa fursa ya kubadilishana uzoefu katika masuala ya utawala na usimamizi wa Rasilimaliwatu kwa kuzingatia shabaha na vipaumbele vya Kitaifa.

Ndugu Washiriki,

Utumishi wa Umma unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutozingatiwa kwa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika kushughulikia masuala mbalimbali ya kiutumishi na menejimenti ya rasilimaliwatu. Kama ambavyo nimekuwa nikiongea mara kwa

mara kuna ukiukwaji mkubwa wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miiko ya kazi katika Utumishi wa Umma vikiwemo utumiaji wa madaraka vibaya, utumiaji vibaya wa mali za Serikali ikiwa ni pamoja na magari ya Serikali, uzembe na usumbufu kwa wananchi ambao ni walipa kodi wanaotufanya tupate mishahara.

Kumbukeni kwamba kazi zinazofanywa na watumishi wa Umma mnaowasimamia ninyi zinaonekana moja kwa moja machoni pa wananchi, hivyo, ukiukwaji unaotendwa na watumishi unaonekana moja kwa moja. Tukumbuke kuwa rasilimali zote husimamiwa na rasilimali watu hivyo ni muhimu kuhakikisha rasilimali watu inasimamiwa vizuri ili iweze kusimamia rasilimali nyingine. Rasilimaliwatu ikisimamiwa vibaya matokeo yake utendaji kazi hushuka, na utendaji kazi ukishuka na uchumi nao hauwezi kukua inavyotakiwa hivyo Taifa kushindwa kufikia malengo yake ya kutoa huduma bora kwa Wananchi.

Ndugu Washiriki,

Suala jingine ambalo ningependa kusisitiza kwenu ni suala la uwajibikaji wenu ninyi Wajumbe wa Kikao hiki. Ninawapongeza wanaofanya vizuri lakini wapo ambao hawawajibiki ipasavyo. Kwa mfano barua nyingi za kuomba ufafanuzi wa masuala mbalimbali zinazojibiwa na Ofisi yangu zinaonesha watu hawawajibiki ipasavyo. Sheria, Kanuni, Taratibu na Nyaraka mbalimbali zipo lakini watu hawazitumii. Badala yake wanapitisha au kuandika barua zije Utumishi ili zifanyiwe kazi ambazo kwa kutumia miongozo niliyoitaja wanapaswa wazishughulikie wao wenyewe. Kwa mfano Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 pamoja na Nyaraka mbalimbali zimeainisha bayana taratibu zinazopaswa kufuatwa katika kushughulikia masuala mbalimbali ambayo ni pamoja na utaratibu wa kuwasilisha mapendekezo ya upekuzi, likizo bila malipo, Ajira za Mikataba, Upandishwaji vyeo kwa utaratibu wa kawaida na mserereko, uhamisho na ubadilishaji kada watumishi.

Badala ya Maafisa husika (yaani ninyi hapa) kuzingatia miongozo iliyopo mnaandika barua Utumishi au mnawashauri vibaya viongozi wenu kuandika barua utumishi kuomba maelekezo na ufafanuzi. Wakati mwingine waajiri wanawasilisha mapendekezo ya kukaimu nafasi za uongozi kwa Maafisa ambao hawana sifa. Hali hii inatoa tafsiri mbili kuwa Wakuu wa Idara za Utawala na Utumishi wanawashauri vibaya Watendaji wakuu ama kwa makusudi au kwa kutowajibika kusoma Miongozo husika. Huku ni kukosa uwajibikaji.

Hali hii ya kutowajibika kwa baadhi ya Wakuu wa Idara za Utawala na Utumishi imejitokeza pia katika zoezi la kuhakiki vyeti vya watumishi ambapo baadhi ya watumishi hawakuhakikiwa vyeti vyao hadi Ofisi yangu ilipotoa maelekezo zaidi ya mara tatu. Vile vile hali hii ilitoa tafsiri mbili ama Wakuu wa Idara za Utawala na Utumishi wana maslahi binafsi na wahusika au hawajali na kufanya kazi kwa mazoea.

Ndugu Washiriki,

Baadhi yenu mnawapandisha vyeo watumishi wakati hawana sifa zilizoainishwa katika Miundo ya Utumishi. Hali hii inawaathiri watumishi husika kwa sababu maombi ya

kubadilisha mishahara ili ilingane na vyeo vipya yasipoidhinishwa na Ofisi yangu, huwashusha ari na morali ya kazi. Nawahimiza Wajumbe wote kuwajibika ipasavyo, kushughulikia na kutoa ufafanuzi wa masuala ya kiutumishi katika maeneo yenu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, na Taratibu badala ya kukiuka au na kuwashauri Waajiri kupitisha barua za kila jambo hata ambalo mna majibu yake.

Ndugu Washiriki,
Viongozi wa ngazi mbalimbali katika Utumishi wa Umma wanakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto kubwa ni ufinyu wa bajeti na hivyo kushindwa kupata vitendea kazi vizuri na kwa wakati. Licha ya changamoto hiyo kubwa, umuhimu wa Wasimamizi wa Rasilimali watu kutekeleza majukumu yao kwa ukamilifu uko pale pale. Kama nilivyosema awali kuwa Rasilimaliwatu ndio inayosimamia Rasilimali nyingine, hivyo ndio msingi mkubwa wa Ufanisi na Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi yoyote kama ilivyowahi kuandikwa na mwanazuoni ajulikanaye kwa jina la Dale Kayser kwamba nanukuu ***"All Management is Human Resources Management"*** mwisho wa kunukuu.

Ndugu Washiriki,
Kutokana na kupewa dhamana ya kutekeleza majukumu hayo ya kusimamia rasilimali hiyo muhimu, Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi anapaswa kuwa na uwezo wa kiuongozi ili kukabiliana na changamoto zilizopo, anapaswa kuwa mbunifu anayeweza kuongoza wakati kunapokuwa na changamoto na anapaswa aone mbali zaidi ya wengine. Huo ndio Uongozi wenyewe.

Ndugu zangu, hatutarajii tuwe na Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi anayetaka kuongoza katika mazingira yasiyo na changamoto kabisa. Hatutarajii Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi kugeuka kuwa mlalamikaji anayetoa lawama kwa Viongozi wengine badala ya kuja na mbinu za kukabiliana na changamoto zilizopo.
Ninapenda kuchukua fursa hii kukutakeni kutumia fursa ya mkutano huu kujadili kwa kina na kubadilishana uzoefu wa namna ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika maeneo yenu. Aidha, ninawataka Wajumbe wote kuwa wabunifu, wazalendo na waadilifu mnapokabiliana na changamoto zilizopo. Ninawaomba muendelee kuwa mahiri katika masuala ya Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa Umma.

Ndugu Washiriki,
Kujenga dhana ya Uongozi wenye heshima na thamani mbele ya unaowaongoza kuna gharama yake. Wala haimaanishi kwamba uwe mtaalam katika kila eneo au katika kila wazo jipya au dhana mpya. La hasha, unachohitaji ni kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sekta unayoisimamia na namna sekta kama yako inavyokwenda mahala pengine *(kujua wengine katika sekta kama yako huko kwingineko wanafanyeje?),* ndipo uweze kuyatafsiri mawazo hayo na kuwasiliana na unaowaongoza kwa lugha nyepesi na njia ambayo wanaweza kuielewa kirahisi ili nyote kwa pamoja muyafikie malengo yenu. Huo ndio Uongozi tunaoutarajia kutoka kwenu na si vinginevyo.

Ndugu Washiriki,
Ninapenda kuwaasa na kuwasisitiza Wakurugenzi wanaosimamia Rasilimaliwatu katika Idara zinazojitegemea, Wakala na Mashirika ya Umma kuwa taasisi zote za Umma zinafanya kazi kwa pamoja na kutekeleza vipaumbele vya Taifa, na sote tunahudumia Umma mmoja wa Watanzania na tunatumia rasilimali za Umma.
Hivyo ninawaagiza kuwashauri Wakuu wa Taasisi zenu na Watumishi mnaowasimamia kuwa na mtazamo huo na kuwaelewesha baadhi ya Viongozi wenu na watumishi kuacha mtazamo wa kuona Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ndio Serikali kwa lugha mnayoitumia ya “Huko Serikalini” na kuona Taasisi zenu kama ni Serikali inayojitegemea. Pia washaurini Viongozi wenu kusimamia Sheria zilizoanzisha Taasisi zenu pamoja na Sheria mama na miongozo mbalimbali inayosimamia Utumishi wa Umma kwa ujumla wake, hili ni **agizo** **na** **si hiari**.

Aidha muwaelimishe watumishi mnaowasimamia kuwa kwa kuwa sote tunahudumia umma wa Watanzania hivyo, wanaweza kuhamishiwa katika Taasisi yoyote ya Umma mathalani Wizarani, Sekretarieti za Mikoa au Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Watumishi wa Wizarani, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaweza kuhamishiwa katika Wakala, Idara zinazojitegemea na Mashirika ya Umma kwa manufaa ya Umma au kwa sababu nyingine kadri itakavyoonekana inafaa.

Ndugu Washiriki,
Ikumbukwe kuwa Katibu Mkuu Utumishi amepewa mamlaka ya kuwahamisha watumishi kutoka kwa Mwajiri mmoja kwenda kwa Mwajiri mwingine ili kuboresha ufanisi na tija katika Utumishi wa Umma. Baadhi ya Waajiri wameanza kujenga tabia ya kukataa kuwaruhusu Watumishi wao kuhama kwa kutopitisha barua na wengine kukataa kuwapokea Watumishi wanaohamishiwa katika Ofisi zao. Ninapenda kuwakumbusha kuwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma Toleo la mwaka 2009, Kanuni C.17 / C.18 Mwajiri haruhusiwi kukataa kupitisha barua iliyoandikwa na mtumishi kwenda kwenye mamkala nyingine bali anapaswa kutoa maoni yake hata kama hakubaliani na maombi husika. Ninawaomba Wajumbe wa kikao hiki kutumia mamlaka na uelewa wenu kuwashauri Viongozi wa Taasisi zenu kuacha tabia hizo.

Ndugu Washiriki,
Suala la Uhamisho wa Watumishi nimekuwa nikilitolea maelekezo mara kwa mara ninapokutana na Watumishi. kwa kuwa leo nimekutana nanyi Viongozi wao, napenda kuliwekea msisitizo tena. Nimekwishaeleza kwa nini Serikali hufanya uhamisho wa Watumishi. Napenda pia muelewe kwamba uhamisho hufanyika kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali. Na kwa mujibu wa miongozo hiyo ni sharti kuwepo na ridhaa ya mwajiri, nafasi wazi ya kujazwa katika kituo kipya na bajeti ya kugharamia uhamisho husika. Aidha, mtumishi anayeomba kuhama anapaswa kuwa amethibitishwa kazini na ametumikia katika kituo hicho kwa muda usiopungua miaka mitatu.

Aidha, kwa kuwa uhamisho wa watumishi wa Umma unaambatana na stahili za kuwezesha uhamisho huo zinazotambuliwa kisheria, ni rai ya Serikali kama ambavyo Rais wetu mpendwa *Dkt.* John Pombe Magufuli amekua akielekeza na kusisitiza mara kwa mara kwamba mtumishi asihamishwe bila kulipwa stahili zake.

Stahili hizi ni kwa ajili ya kumwezesha mtumishi kutekeleza uhamisho unaofanywa bila ya matakwa yake pamoja na kufidia usumbufu unaotokea katika kufungasha mizigo na kusafirisha familia yake. Na kwa kuwa hatutaki kuongeza limbikizo la madeni, na mimi naomba nikazie hapohapo, Waajiri msiwahamishe wala kuwaombea uhamisho watumishi bila kuwa na uhakika wa fedha za kugharamia uhamisho huo. Na iwapo mtumishi atakuletea maombi ya kuhamishwa, basi katika maombi yake ni sharti athibitishe utayari wa kujigharamia kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni L.8 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009;

Ndugu Washiriki,
Tafiti zinatuonesha kwamba wengi wenu hampendi kujishughulisha kuisoma ama kuifuata miongozo inayotolewa na Serikali. Badala yake kila mmoja anajifanyia vile ambavyo utashi wake unavyomsukuma kutenda. Jambo hili limetuletea migogoro mingi ndani ya Utumishi wa Umma. Napenda kutumia hadhara hii kuwakumbusha kuwa Mtumishi yeyote wa Umma anatakiwa kuwa na Nyaraka muhimu za Utendaji kazi mezani kwake ambazo zinamuongoza katika kupanga mikakati ya kutekeleza majukumu yake. Nyaraka hizo pamoja na zile za kitaalamu kulingana na kada yako, ni Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, Mpango Mkakati wa Taasisi (Strategic Plan) na Mpango kazi.

Ndugu Washiriki,
Kabla sijaendelea sana na hotuba yangu, naamini sote tunatambua lakini si vibaya tukakumbushana kwamba nchi yetu iko katika Mfumo wa Vyama vingi vya siasa. Mtumishi hakatazwi kuwa mwanachama wa chama chochote cha Siasa. Lakini ikumbukwe kuwa Watumishi wa Umma wanapaswa kutii Serikali iliyopo madarakani kwa wakati uliopo na kutekeleza Ilani yake.

Ndugu Washiriki,
Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala – (CCM) ya Mwaka 2015 imeweka malengo ya kuitoa nchi yetu kutoka kuwa na uchumi ulio nyuma na tegemezi kuelekea uchumi wa Viwanda kwa kuzingatia vipaumbele mbalimbali. Ninapenda kuwakumbusha utekelezaji wa Ilani hii ya Uchaguzi ya Chama Tawala kwa kiasi kikubwa unawategemea watumishi wa Umma ambao ninyi mnawasimamia. Kumekuwepo na tabia kwa baadhi ya watumishi kuwa kikwazo kwa Serikali katika kutekeleza majukumu yake kwa kuvujisha siri za Serikali kwa vyombo vya habari na kwa watu wasiohusika kwa lengo la kuichafua Serikali. Ninawaasa mwende mkasimamie na kuhakikisha kuwa watumishi wote

wanatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2015 na wanatoa huduma kwa usawa bila upendeleo wa aina yoyote ile.

Ndugu Washiriki,
Ninapenda kuwakumbusa na kusisitiza rai ya utendaji kazi na uwajibikaji wa Watumishi wa Umma aliyotoa Rais wetu Mpendwa Mhe. *Dkt.* John Pombe Joseph Magufuli wakati akifungua rasmi Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma, tarehe 20 Novemba 2015, nanukuu "***Natoa rai kwa watumishi wa serikali, hasa ambao ni wazembe na wavivu, kujiandaa. Wamevumiliwa kwa muda mrefu sasa basi. Kwa sababu watumishi wa aina hiyo hawatavumuliwa katika serikali nitakayoiongoza. Mimi nataka watu wa Kazi Tu. Hatuwezi kulea watu ambao wanalipwa mishahara lakini hawafanyi kazi wanazotakiwa kufanya, au wamegeuza Ofisi za umma kuwa ni mahala pa kuchuma bila kufanya kazi"*** mwisho wa kunukuu.

Sasa naomba niwaulize ninyi Wasimamizi wa Rasilimaliwatu, hivi watumishi wazembe, walevi, wasiojali hamuwaoni au hawapo? Ni wangapi mmewachukulia hatua? Ninawaagiza mkawashauri Waajiri wenu kuchukuwa hatua za kinadhamu mara moja kwa watumishi wa aina hiyo, simamieni maadili na Mifumo yote ya kuboresha utendaji kazi mathalani OPRAS na Mkataba wa Huduma kwa Mteja ili kuhakikisha watumishi wote wanawajibika na kulipwa mishahara kwa kazi zenye matokeo na tija kwa wananchi.

Ndugu washiriki*,*
Nimearifiwa kwamba katika Mkutano huu mada zifuatazo zitawasilishwa:-

- Wajibu na majukumu ya Mkuu wa Idara ya Rasilimali watu
- Masuala muhimu katika Usimamizi wa Utumishi wa Umma na marekebisho muhimu ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma
- Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma
- Usimamizi wa Usalama wa Nyaraka na Mali za Serikali
- Changamoto za Utendaji kazi kutoka OR – MUUUB
- Changamoto za Utendaji kazi kutoka kwa Wajumbe
- Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii
- Usimamizi wa Mashirika ya Umma

Nawapongeza waandaaji kwa kuwaandalia mada ambazo kimsingi zinagusa karibia maeneo mengi muhimu. Ni matumaini yangu kuwa mada hizo zitawawezesha Wajumbe kupata uelewa wa Taratibu mbalimbali zinazopaswa kuzingatiwa katika utendaji wa kazi kama zilivyoainishwa kwenye Sheria, Kanuni, Taratibu na Nyaraka mbalimbali zinazotolewa katika Utumishi wa Umma na kwenda kuzitelekeza kwa vitendo. Pia nitumie fursa hii kuwasihi wajumbe wa kikao kuichukulia kila mada kwa uzito kabisa bila ulegevu.

Ndugu Wajumbe,
Mwisho kabisa, lakini si mwisho kwa umuhimu niwakumbusheni kuhusu uzingatiaji wa Maadili ya Utumishi wa Umma kama Viongozi. Kiongozi unapaswa kuwa mfano kwa tabia njema, kupinga rushwa na kuzingatia maadili ya Uongozi kwa ujumla. Rushwa ni adui wa haki, ukiwa Kiongozi jukumu lako kubwa ni kusimamia haki. Lakini usipojiepusha na rushwa huwezi kutenda haki kwa unaowaongoza na zaidi sana utaishia kuhujumu rasilimali za nchi. Wewe utakua msaliti miongoni mwetu, hauna tofauti na abiria anayetoboa mtumbwi katikati ya safari, hatuwezi kukuvumilia ni lazima tukutose majini ili tuendelee na safari na kuweza kufika salama huko tuendako.

Katika maeneo yenu ya kazi, limekuwa jambo la kawaida kukuta baadhi yenu kwa waziwazi au kwa kificho kupitia makampuni yenu au ya jamaa zenu, mmekuwa mkifanya biashara na Taasisi zenu. Jambo hili limepelekea kuwepo kwa mgongano wa maslahi na kuisababishia Serikali hasara kubwa. Huwezi kuwa hakimu wa kesi yako mwenyewe na bado ukatenda haki. Nyie wenyewe mnashiriki kwenye vikao vya tenda, nyie wenyewe mnataka kupewa tenda, haki itatendeka hapo kweli? Haiwezekani!

Huenda mnayafanya haya kwa makusudi au kwa sababu ya kukosa uelewa. Kwa sehemu kubwa tabia hii inachangiwa na kutotelekeza miongozo na maelekezo mbalimbali yanayotolewa mara kwa mara na Serikali.
Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwishatoa maelekezo ya kuwataka waajiri wote kuwaalika TAKUKURU na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kila mnapokuwa na mkusanyiko wa Watumishi katika maeneo yenu ya kazi ili waweze kutoa mada. Iwe Baraza la Madiwani, Baraza la Wafanyakazi au Mikutano mingine mnapaswa kuwaalika wataalamu hawa ili wawapeni elimu kuhusu Maadili na mapambano dhidi ya rushwa katika utekelezaji wa majukumu yenu ya kila siku. Tafadhali lizingatieni hilo na pendeni kujielimisha mara kwa mara ili kuisoma vizuri dira na kuendana na kasi ya Awamu ya Tano.

Ndugu Wajumbe,
Kazi kubwa niliyopewa kwa siku ya leo ni kufungua Kikao, lakini nimeona niseme nanyi mambo machache kati ya mengi niliyonayo. Si lengo langu kuwafilisi watoa mada mtakaokuwa nao kwa siku mbili za Kikao hiki maana ninaamini mtayazungumza, mtayajadili na kufundana ipasavyo kwa maslahi mapana ya Nchi yetu.

Baada ya kusema hayo sasa nachukua fursa hii kutamka kwamba **Kikao Kazi cha Wakuu wa Idara za Utawala na Rasilimaliwatu katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kimefunguliwa rasmi** na ninakutakieni majadiliano mazuri.

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA